## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



# MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA

OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU
TAKWIMU
TANZANIA
TAKWIMU KWA MAENDELEO

**Novemba, 2023**

## YALIYOMO

DIBAJI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ii
1 DIRA, DHIMA, NA MAADILI YETU 1
1.1 Dira 1
1.2 Dhima 1
1.3 MAADILI YETU 1
2 DHUMUNI LA MKATABA 1
3 WATEJA NA WADAU WETU 2
3.1 Bidhaa na Huduma zetu 2
4 WAJIBU 8
5 HAKI NA WAJIBU WA MTEJA. 8
5.1 Haki za Mteja: 8
5.2 Wajibu wa Mteja: 8
6 MAONI YA WATEJA NA USHUGHULIKIAJI MALALAMIKO 9
7 SAA ZA KAZI NA MAWASILIANO 10
7.1 Saa za Kazi 10
7.2 Mawasiliano Yetu 10

## DIBAJI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

Ndugu Wateja na Wadau wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ninayo furaha kuwasilisha kwenu Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa NBS unaoonesha dhamira ya NBS ya kuongeza upatikanaji wa takwimu rasmi zenye ubora kwa ajili ya kufanya maamuzi ndani ya serikali, sekta binafsi, jumuiya ya kimataifa na umma kwa ujumla.

Mkataba huu ukiwa ni wa kijamii kati ya NBS na wateja wake, unaeleza dhamira ya taasisi katika kutoa bidhaa na huduma bora, na kubainisha kile ambacho mteja anakitarajia anapokuja NBS kwa ajili ya kupata huduma za kitakwimu na zinazohusiana nazo. Mkataba unabainisha bidhaa na huduma zitolewazo na viwango vyake.

Kwa hivyo, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itashukuru kupata maoni kutoka kwa wateja wake kuhusu jinsi inavyotoa huduma zake kulingana na viwango vilivyoainishwa. Maoni haya ni muhimu, kwa kuwa yatatumika kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma kila mara pamoja na ubora wa bidhaa za takwimu zinazozalishwa.

Ningependa kuwahakikishia wateja wetu wote kuwa NBS itazingatia viwango vya takwimu na huduma vilivyotajwa katika Mkataba huu na kuwafahamisha yale yote yanayohusu takwimu rasmi na huduma nyingine zinazotolewa na NBS.

Dkt. Albina Chuwa

**Mtakwimu Mkuu wa Serikali**

# 1 DIRA, DHIMA, NA MAADILI YETU

Katika kutoa huduma, NBS inaongozwa na Dira, Dhamira na Maadili ya Msingi yafuatayo:-

## 1.1 Dira

*Kuwa kitovu cha takwimu rasmi Tanzania*

## 1.2 Dhima

*Kutoa takwimu rasmi zilizo bora na huduma zinazokidhi mahitaji ya wadau wa kitaifa na kimataifa kwa ajili ya kupanga mipango na kufanya maamuzi yenye uthibitisho*

## 1.3 Maadili yetu

Maadili yetu ya msingi ni:

i. Kujali Wateja;
ii. Kufanya Kazi Pamoja;
iii. Uadilifu;
iv. Usiri;
v. Ushirikiano;
vi. Utendaji Wenye Matokeo;
vii. Dhamira ya Ubora;
viii. Weledi;
ix. Uwajibikaji; na
x. Ubunifu.

# 2 DHUMUNI LA MKATABA

Dhumuni la Mkataba huu ni kuwafahamisha wateja na wadau wetu kuhusu bidhaa na huduma za kitakwimu zinazopatikana; pamoja na viwango vya bidhaa na huduma hizo. Mkataba unaonesha dhamira yetu katika kufikia matarajio ya kukidhi mahitaji ya wateja na wadau wetu ili kuwezesha ofisi kuzalisha bidhaa na huduma zenye viwango. Aidha, Mkataba unatoa mfumo wa namna ya wateja na wadau wetu kutoa maoni na mrejesho ili kuimarisha ushirikiano kati yao na NBS.

# 3 WATEJA NA WADAU WETU

Wateja na wadau wetu ni pamoja na : -

i. Wizara, Idara na Wakala wa Serikali;
ii. Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI);
iii. Washirika wa Maendeleo;
iv. Bunge;
v. Mahakama;
vi. Taasisi za Elimu, Utafiti na Mafunzo;
vii. Jumuiya za Kikanda: (Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU);
viii. Asasi za Kiraia;
ix. Sekta Binafsi;
x. Wanasiasa;
xi. Jumuiya ya Wafanyabiashara;
xii. Vyombo vya Habari; na
xiii. Umma kwa ujumla

## 3.1 Bidhaa na Huduma zetu

Tunatoa bidhaa na huduma zifuatazo:-

i. Takwimu za Kiuchumi;
ii. Takwimu za Kijamii;
iii. Takwimu za Mazingira;
iv. Uratibu wa Takwimu, Viwango na Mbinu za Kitakwimu;
v. Ushauri wa Kitakwimu;
vi. Huduma za Maktaba ya Takwimu; na
vii. Huduma ya Kumbi za Mikutano.

## Viwango vya Bidhaa/Huduma zetu

| Na. | Kitengo cha Bidhaa/Huduma | Kitengo kidogo cha Bidhaa/Huduma | Na. | Bidhaa/Huduma | Muda | Muda wa Kutoa Bidhaa/Huduma |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Takwimu za Kijamii | Ripoti | i. | Ripoti za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi | Kila baada ya Miaka mitano (5) | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | ii. | Ripoti za Sensa ya Watu na Makazi | Kila baada ya Miaka 10 | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | iii. | Ripoti ya Utafiti wa Tathmini ya Utoaji wa Huduma za Afya Tanzania (TSPA). | Kila baada ya Miaka mitano (5) | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | iv. | Ripoti za Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria | Kila baada ya Miaka mitano (5) | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | v. | Ripoti za Utafiti wa Athari za Virusi Vya Ukimwi Tanzania | Kwa vipindi visivyo maalumu | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | vi. | Ripoti za Utafiti wa STEPs | Kwa vipindi visivyo maalumu | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | vii. | Ripoti ya Takwimu za Makazi | Kila Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | viii. | Ripoti ya Takwimu za Mazingira | Kila baada ya Miaka miwili (2) | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | ix. | Chapisho la Takwimu za Kitaifa za Mabadiliko ya Tabianchi | Kwa vipindi visivyo maalumu | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |

| Na. | Kitengo cha Bidhaa/Huduma | Kitengo kidogo cha Bidhaa/Huduma | Na. | Bidhaa/Huduma | Muda | Muda wa Kutoa Bidhaa/Huduma |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | x. | Ripoti ya Kitakwimu ya Taka za Kielektroniki | Kila baada ya Miaka miwili (2) | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | Fremu ya Sampuli | 1 | Sampuli Kuu ya Kitaifa | Kila baada ya miaka 10 | Ndani ya siku saba baada ya kupokea maombi |
| 2. | Takwimu za Kiuchumi | Ripoti | i. | Wasifu wa Kiuchumi wa Kijamii wa Mikoa na Wilaya | Inapohitajika | Ndani miezi mitatu kutegemea uwepo wa nyezo |
| | | | ii. | Makadirio ya Pato la Taifa | Kila Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | iii. | Makadirio ya Pato la Taifa | Robo Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | iv. | Takwimu za Ukuzaji Rasilimali | Kila Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | v. | Ripoti ya Utafiti wa Wageni wa Kimataifa | Kila Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | vi. | Fahirisi ya Bei ya Mtayarishaji (PPI). | Robo Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | vii. | Utafiti wa Takwimu za Uzalishaji Viwandani | Kila Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | viii. | Farihisi za Uzalishaji Viwandani (IIP) | Robo Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | ix. | Ripoti ya Sampuli ya Sensa ya Kilimo | Kila baada ya Miaka Mitano (5) | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | x. | Ripoti ya Utafiti wa Kilimo Jumuishi | Kila Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | xi. | Ripoti ya Uwekezaji wa Kibinafsi wa Kigeni | Kila Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |

| Na. | Kitengo cha Bidhaa/Huduma | Kitengo kidogo cha Bidhaa/Huduma | Na. | Bidhaa/Huduma | Muda | Muda wa Kutoa Bidhaa/Huduma |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | xii. | Takwimu za Biashara ya Uagizaji na Uuzaji wa Bidhaa Nje ya Nchi | Inapohitajika | Ndani ya siku tatu (3) za kazi |
| | | | xiii. | Fahirisi za Bei ya Biashara | Robo Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | xiv. | Machapisho ya Takwimu ya Pato la Taifa | Kila Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | xv. | Ripoti ya Sensa ya Viwanda | Kila baada ya Miaka 10 | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | xvi. | Ripoti ya Takwimu za Kodi | Kila mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | xvii. | Ripoti ya Utafiti wa Uzalishaji wa Mashamba Makubwa | Kila mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | xviii. | Fahirisi ya Bei ya Vifaa vya Ujenzi | Kila mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | xix. | Farihisi za Bei za Taifa | Kila Mwezi | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | xx. | Ripoti ya Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi | Episodic | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | xxi. | Ripoti ya Takwimu za Ajira na Mapato | Kila Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | xxii. | Ripoti ya Utafiti Jumuishi wa Biashara | Episodic | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | xxiii. | Ripoti Jumuishi ya Utafiti wa Nguvu Kazi | Kila Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | Taarifa | i. | Taarifa ya Takwimu za Hoteli | Kila Mwezi | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | | ii. | Taarifa ya Mfumuko wa Bei | Kila Mwezi | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |

| Na. | Kitengo cha Bidhaa/Huduma | Kitengo kidogo cha Bidhaa/Huduma | Na. | Bidhaa/Huduma | Muda | Muda wa Kutoa Bidhaa/Huduma |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *Economic accounting* | 1 | Bangokitita la Shughuli za Kiuchumi | Kila baada ya miaka mitano (5) | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya NBS) |
| | | Majedwali | 1 | Majedwali ya Hali ya Uchumi | Kila mwaka | Ndani ya siku tatu (3) za kazi. |
| 3. | Uratibu viwango na mbinu. | Ripoti | i. | Viashiria vya Uchumi wa Kijamii | Kila mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.) |
| | | | ii. | Ripoti ya Takwimu za Msingi Tanzania | Kila mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.) |
| | | | iii. | Muhtasari wa Takwimu za Msingi Tanzania | Kila mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.) |
| | | | iv. | Ramani za Kijiografia za Sensa | Inapohitajika | Ndani ya siku tatu (3) za kazi kabla ya malipo ya ada. |
| | | | v. | Ripoti ya Takwimu Muhimu za Afrika Mashariki *(EAC Facts and Figures Report)* | Kila Mwaka | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.) |
| | | | vi. | Daftari la Usajili wa Takwimu za Biashara. | Kila baada ya miaka mitatu (3) | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.) |
| | | Miongozo | i. | Dhana ya Ufafanuzi wa Takwimu Rasmi Nchini. | Kila baada ya miaka mitatu (3) | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.) |
| | | | ii. | Mfumo wa Tathmini wa Ubora wa Data | Kila baada ya miaka mitano (5) | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.) |
| | | | iii. | Mwongozo wa Mbinu na Viwango vya Machapisho ya Kitakwimu | Kila baada ya miaka mitano (5) | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.) |

| Na. | Kitengo cha Bidhaa/Huduma | Kitengo kidogo cha Bidhaa/Huduma | Na. | Bidhaa/Huduma | Muda | Muda wa Kutoa Bidhaa/Huduma |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | Kalenda Kuu ya Motoleo ya Takwimu Rasmi Nchini | Kila baada ya miaka mitano (5) | Papo hapo (inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.) |
| 4. | Ushauri wa kitakwimu | [Uandaaji wa] Sampuli | i. | Uandaaji wa sampuli | Inapohitajika | Ndani ya siku tano (5) za kazi kulingana na asili na mawanda ya utafiti. |
| | | [Uandaaji wa] Dodoso/Madodoso | ii. | Uandaaji wa dodoso/madodoso | Inapohitajika | Ndani ya siku tano (5) za kazi. |
| | | Utafiti | iii. | Kufanya tafiti | Inapohitajika | Kulingana na asili na mawanda ya utafiti /sensa |
| | | [Ukusanyaji wa] Data | iv. | Kukusanya data | Inapohitajika | Kulingana na asili na mawanda ya utafiti /sensa |
| | | Sensa | v. | Kufanya Sensa | Inapohitajika | Kulingana na asili na mawanda ya utafiti /sensa |
| 5. | Vibali vya utafiti | Vibali | 1 | Kutoa vibali vya tafiti | Inapohitajika | Ndani ya siku tano (5) za kazi. |
| 6. | Huduma nyinginezo | Huduma ya Maktaba | i. | Huduma ya maktaba | Inapohitajika | Inapatikana muda wa saa za kazi |
| | | Huduma za mkutano | ii. | Kutoa huduma za mikutano | Inapohitajika | Mara moja ikiwa haijashughulikiwa. |

## 4 WAJIBU

Katika mchakato wa kukidhi mahitaji ya wateja, wajibu wetu ni: -

i. Kutoa bidhaa na huduma kwa mujibu wa viwango na vilivyobaliwa na kuidhinishwa katika Mkataba huu;
ii. Usiri wa taarifa za mteja;
iii. Kutoa huduma kwa misingi ya uwazi na usawa.
iv. Kuheshimu mawazo na maoni ya wateja;
v. Kutoa huduma zinazokidhi mahitaji ya wateja;
vi. Kutumia lugha rahisi wakati wa kuhudumia wateja;
vii. Kujibu barua za wateja ndani ya siku saba (7) za kazi baada ya kupokelewa;
viii. Kujibu barua pepe ndani ya siku tano (5) za kazi baada ya kupokelewa;
ix. Kujibu simu zinazoingia ndani ya miito mitano (5) siku za kazi;
x. Kujibu maswali ya wateja ndani ya siku tano (5) za kazi baada ya kuyapokea;
xi. Kusambaza matokeo na matokeo ya Sensa na tafiti kwa wakati; na
xii. Kueleza na kutangaza huduma zinazotolewa na ofisi ya Taifa ya Takwimu

## 5 HAKI NA WAJIBU WA MTEJA.

### 5.1 Haki za Mteja:

i. Kupewa bidhaa na huduma bora za kitakwimu kwa wakati;
ii. Kupewa taarifa zisizo na upendeleo;
iii. Kuomba na kupewa taarifa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa;
iv. Kupewa nafasi ya kuwasilisha malalamiko, maoni na mapendekezo kuhusu huduma zilizopokelewa;
v. Kujulishwa, ndani ya siku tano (5) za kazi, kupokelewa kwa malalamiko aliyowasilisha; na
vi. Kupewa, ndani ya siku thelathini (30), majibu ya malalamiko aliyowasilisha kwa njia ya maandishi kulingana na aina ya malalamiko.

### 5.2 Wajibu wa Mteja:

Ili tuweze kutekeleza majukumu yetu kwa haraka na ufanisi, tunatarajia mambo yafuatayo kutoka kwa wateja wetu:-

i. Kuwaheshimu wafanyakazi wetu;
ii. Kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu zilizopo;

iii. Kuhudhuria mikutano iliyopangwa au miadi kwa wakati;
iv. Kutoa taarifa sahihi na kwa wakati ili kuwezesha utoaji sahihi wa huduma;
v. Kujibu maswali mara moja;
vi. Kutoa mrejesho na maoni kuhusu huduma zinazotolewa na NBS;
vii. Kulipia huduma maalum zinazotolewa na NBS; na
viii. Kutoa taarifa/majibu sahihi anapotakiwa wakati wa tafiti za kitakwimu.

# 6 MAONI YA WATEJA NA USHUGHULIKIAJI MALALAMIKO

Ofisi ya Taifa ya Takwimu inathamini maoni yako kuhusu bidhaa na huduma za kitakwimu na zisizo za takwimu inazozitoa. Maoni yako yatashughulikiwa kwa usiri wa hali ya juu na kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa pekee. Tafadhali toa maoni yako kupitia simu, barua pepe, sanduku la maoni, tovuti au kwa kutembelea Makao Mkuu ya NBS na Ofisi zetu za Takwimu za Mikoa zinazopatikana katika kila makao makuu ya mkoa.

**Mapitio ya Mkataba**

Mkataba huu utapitiwa upya kadiri itakavyohitajika

# 7 SAA ZA KAZI NA MAWASILIANO

## 7.1 Saa za Kazi

Huduma zetu kwa wateja zinapatikana kuanzia saa 01:30 Asubuhi hadi saa 9:30 Alasiri kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za mapumziko na sikukuu.

## 7.2 Mawasiliano Yetu

Unaweza kuwasiliana na ofisi yetu kwa anuani zifuatazo:

Mtakwimu Mkuu wa Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Takwimu,
TAKWIMU HOUSE,
64 Lusinde Road,
S.L.P 2683,
41101 Tambukareli – **DODOMA. Tanzania**
Simu +255 26 2963822; Nukushi: +255 26 2963828
Barua Pepe: sg@nbs.go.tz; Tovuti: www.nbs.go.tz

## Ofisi za Takwimu za Mikoa - Tanzania Bara

| Na. | Mkoa | Anuani | Simu ya Ofisi | Barua Pepe | Simu za Mameneja Takwimu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | S.L.P 7108 | +255 27 2502009 | rsmarusha@nbs.go.tz | 0676 919 355 |
| 2 | Dodoma | S.L.P 891 | +255 26 2963133 | rsmdodoma@nbs.go.tz | 0754 697 765/ 0784 697 765 |
| 3 | Morogoro | S.L.P 581 | +255 23 2604974 | rsmmorogoro@nbs.go.tz | 0657 343 054 |
| 4 | Pwani | S.L.P 30080 | +255 23 2402275 | rsmpwani@nbs.go.tz | 0762 022 870 |
| 5 | Tanga | S.L.P 566 | +255 27 2646332 | rsmtanga@nbs.go.tz | 0713 755 965 |
| 6 | Mara | S.L.P 769 | +255 28 2622447 | rsmmara@nbs.go.tz | 0785 380 083 |
| 7 | Ruvuma | S.L.P 397 | +255 26 2602449 | rsmruvuma@nbs.go.tz | 0759 603 045/ 0655 586 516 |
| 8 | Mtwara | S.L.P 56 | | rsmmtwara@nbs.go.tz | 0713 547 488 |
| 9 | Rukwa | S.L.P 797 | +255 25 2802771 | rsmrukwa@nbs.go.tz | 0754 605 810 |
| 10 | Lindi | S.L.P 506 | +255 23 2202680 | rsmlindi@nbs.go.tz | 0719 398 467 |
| 11 | Manyara | S.L.P 89 | +255 27 25110097 | rsmmnyara@nbs.go.tz | 0767 078 971 |
| 12 | Iringa | S.L.P 739 | +255 26 2702771 | rsmiringa@nbs.go.tz | 0752 202 726/ 0655 202 726 |
| 13 | Shinyanga | S.L.P 2134 | +255 28 2762901 | rsmshinyanga@nbs.go.tz | 0755799252 |
| 14 | Mwanza | S.L.P 1932 | +255 28 2502500 | rsmmwanza@nbs.go.tz | 0713356969 |
| 15 | Kagera | S.L.P 1299 | +255 28 2220836 | rsmkagera@nbs.go.tz | 0656 555 931/ 0713 495 669 |
| 16 | Njombe | S.L.P 739 | +255 26 2702771 | rsmnjombe@nbs.go.tz | 0712 199 007 |
| 17 | Singida | S.L.P 807 | +255 26 25028120 | rsmsingida@nbs.go.tz | 0713 481 044/ 0787 207 470 |
| 18 | Kigoma | S.L.P 953 | +255 28 2803360 | rsmkigoma@nbs.go.tz | 0756 627 828 |
| 19 | Mbeya | S.L.P 841 | +255 252502612 | rsmmbeya@nbs.go.tz | 0719 280 135 |
| 20 | Simiyu | S.L.P 2134 | +255 28 2762901 | rsmsimiyu@nbs.go.tz | 0656 883 424/ 0783 954 990 |
| 21 | Tabora | S.L.P 703 | +255 26 2605202 | rsmtabora@nbs.go.tz | 0784 242 020 |
| 22 | Geita | S.L.P 1932 | +255 28 2502005 | rsmgeita@nbs.go.tz | 0784 585 083/ 0752 145 263 |
| 23 | Katavi | S.L.P 797 | +255 25 2820626 | rsmkatavi@nbs.go.tz | 0753 651 927 |
| 24 | Dar es Salaam | S.L.P 796 | | rsmdsm@nbs.go.tz | 0768 202 040 |
| 25 | Kilimanjaro | S.L.P 1 | +255 27 2751662 | rsmkilimanjaro@nbs.go.tz | 0719 491 949/ 0764 530 537 |
| 26 | Songwe | S.L.P 7108 | | rsmsongwe@nbs.go.tz | 0717 062 916 |